

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO  
MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**



**MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA ASEPTEMBER, 2018 NA  
MWELEKEO WA OKTOBA, 2018**

**Dondoo za Septemba, 2018.**

Taarifa hii inatoa muhtasari wa mifumo ya hali ya viashiria pamoja na mwenendo wa mvua kwa mwezi Septemba, 2018 na mwelekeo wa viashiria pamoja na hali ya joto kwa mwezi Oktoba, 2018 nchini.

- a) Kwa mwezi Septemba, 2018 vipindi vifupi vya mvua nyepesi vilijitokeza katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa Pwani na ukanda wa ziwa Victoria, na maeneo mengine ya nchi yaliyosalia yaliendelea kuwa makavu kwa ujumla.
- b) Katika kipindi cha mwezi Oktoba, 2018, vipindi vya mvua vinatarajiwa kuendelea katika maeneo ya ukanda wa ziwa Victoria pamoja na maeneo ya ukanda wa Pwani. Vile vile vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo ya Nyanda za Juu Kaskazini Mashariki.

**1. MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI  
SEPTEMBER, 2018 NA MATAZAMIO YA MWEZI OKTOBA, 2018**

**1.1. MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI  
SEPTEMBER, 2018**

Katika kipindi cha mwezi Septemba, 2018 vipindi vya mvua vimejitokeza katika baadhi ya maeneo ya ukanda ya ziwa Victoria na Pwani ya Kaskazini kama vilivyotabiriwa, hata hivyo vipindi kadhaa vya mvua za nje ya msimu pia vimejitokeza katika baadhi ya maeneo ya Pwani ya kusini.

**2.0 MATAZAMIO KWA MWEZI OKTOBA, 2018**

**2.1 MIFUMO YA HALI YA HEWA**

Hali ya joto la bahari la juu ya wastani inatarajiwa katika maeneo ya kati ya Kitropiki ya Bahari ya Pasifiki, kusini magharibi mwa bahari ya Hindi, pwani ya Somalia pamoja na kaskazini mwa Bahari ya Hindi ilihali joto la chini ya wastani inatarajiwa katika maeneo ya pwani ya Angola katika kipindi cha mwezi Oktoba, 2018. Hali hii ya joto la juu ya wastani kakika maeneo ya

Pwani ya Somalia na Kaskazini ya bahari ya Hindi inatarajiwa kusababisha ukanda wa mvua kushuka taratibu zaidi kutoka katika pembe ya Afrika hivyo kusababisha mtawanyiko hafifu wa mvua za Vuli katika baadhi ya maeneo nchini.

## **2.2 HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI OKTOBA, 2018**

Ufuatao ni mwelekeo wa hali ya hewa nchini;

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba):** Vipindi vya mvua nyepesi vinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo katika wiki mbili za mwanzo wa mwezi, na baadaye ongezeko la vipindi vya mvua katika wiki zilizosalia za mwisho wa mwezi.

**Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara):** Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa kuendelea katika kipindi cha wiki mbili za mwanzo wa mwezi ikifuatiwa na vipindi vya mvua katika wiki mbili zilizosalia za mwezi.

**Kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu):** Vipindi vya mvua nyepesi vinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo ya kanda ya ziwa katika kipindi cha wiki mbili za mwanzo wa mwezi Oktoba na baadae ongezeko la mvua linatarajiwa katika kipindi cha mwezi kilichosalia.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):** Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa kuendelea.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):** Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa kuendelea.

**Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Njombe, Iringa na Mbeya):** Hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):** Vipindi vya ukavu vinatarajiwa katika wiki tatu za mwanzo wa mwezi vikifuatiwa na vipindi vya mvua nyepesi katika wiki ya mwisho wa mwezi zilizosalia.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma):** Hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea.

Imetolewa na;

**MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**